**Maswali na Majibu**

1. Tunatakiwa tufanye nini baada ya kubatizwa?
   *Tubadilishe maisha yetu*
2. Tunatakiwa tufanye nini ili tukue kama watoto wa Mungu?
   *Kusoma neno lake na kuomba kila siku.*
3. Watu watajuaje kwamba sisi tu watu tofauti?
   *Kupitia kwa mwienendo yetu*
4. Orodhesha viwango 9 vya tunda la roho.
   *Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, imani, upole, kiasi.*
5. Yesu alisema amri kuu ni gani? *Upendo.*
6. Mbona tumpende Mungu kwa hali zote?
   *Kwa sababu Mungu ametuonyesha upendo mwingi kwa kutupea mwanawe wa pekee.*
7. Watu 3 walionyesha furaha katika mateso yao ni nani?
   *Paulo na Sila na Yesu.*
8. Tunaweza kuonyesha uvumilivu namna gani tukiteswa?
   *Kwa kuvumilia tukitarajia tukingoja Ufalme.*
9. Tunaweza kurahihisha kuwa wema kwa watu namna gani?
   *Tukiangalia hali ya maisha na tuwaelewe zaidi.*
10. Tunda la roho ni nini?
    *Tabia za Mungu kukua ndani ya maisha ya watoto Wake.*

## Mistari ya kukariri

Waebrania 4:16; Wagalatia 5:22 – 23; Wafilipi 4:8; 1 Wakorintho 13:4 – 8.

## Mazungumzo

Soma 1 Wakorintho 13:4 – 8 yote. Zungumza ni kipengele gani kigumu kutimiza. Sema vile unaweza kufaulu.

## Kuandika

Taja viwango 9 vya tunda la roho. Andika sentensi kwa kila moja yao vile unaweza kuonyesha kwa maisha yako.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 46 Maisha mapya katika Kristo

**SOMA Waebrania 4:16; Wagalatia 5:22 – 23; Yohana 15:5; 1 Wakorintho 13:4 – 8; Wafilipi 4:8**

**SOMO**

Tukisha batizwa tunaanza maisha mapya. Maisha tuliyokuwa tukiishi inaishia pale. Tukitoka, inje ya maji ya ubatizo tunaanza maisha mapya katika Kristo. Haya mabadiliko ya maisha yatawezekana kwa usaidizi wa Mungu. Vile tutakuwa tukijaribu kumpendeza Mungu, tutakuwa tukikoza, lakini tunaomba msamaha, Atatusikia kwa minajili ya Yesu.

Chakula ni cha maana ili mtoto akue. Tukizaliwa kwa maisha mapya kama watoto wa Mungu, tutakua ikiwa tutakula neno la Mungu. Tunatakiwa tusome na tutafakari juu ya neno la Mungu kila siku. Tunatakiwa tuzungumze na Mungu katika maombi.

Yesu aliambia wanafunzi wake kwamba yeye ni kama mzabibu na wao ni matawi. Matawi yanaweza kuzaa matunda, ikiwa yanakua juu ya mti yakila uzuri kutoka kwa mti. Tawi lisipojishikilia kwa mti, haliwezi kuzaa matunda. Matunda huwa yanaonyesha mfano wa mti yanayotoka. Hata na sisi, tabia zetu zinaonyesha tu watu wa aina gani. Tunatakiwa tuwe karibu na Yesu ili tukue kama yeye na tuonyeshe tunda la roho wa Mungu kwa maisha yetu.

Wagalatia 5:22 – 23 inatwambia juu ya tunda la roho linalotakiwa likue ndani ya maisha yetu. Tunda la roho ni tabia za Mungu zenye Yesu alikuja kuonyesha katika maisha yake. Tunda la roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili (uzuri), uaminifu, upole, kiasi. Kwa maisha yetu mapya tunatakiwa tuwe na haya matunda katika Kristo. Si rahisi kuwa na tabia za Mungu kwa maisha yetu. Tunatakiwa tuombe usaidizi Wake.

Hebu tuangalie kila tunda na tufikirie vile tunaweza kuweka kwa vitendo.

**Upendo**

Yesu alisema kwamba upendo ndiyo amri kuu. Alisema lazima tupende Mungu na jirani wetu. Soma 1 Wakorintho 13:4 – 8.

Upendo ni msingi wa ujumbe wa Injili na inatakiwa iwe katika maisha ya mwumini. Yesu alisema kwamba amri kuu ni kupenda Mungu na moyo wako wote, nafsi yako na mawazo yako yote – katika hali yote.

Mungu ametuonyesha upendo mwingi. Alituma Mwanawe wa pekee, aliyempenda katika ulimwengu kutoa uhai wake ili tuokoke. Yesu aliishi na akafa kwa ajili yetu kwa sababu alitupenda. Alipeana uhai wake kuokoa wenye dhambi kama sisi. Mungu alitupenda hata kama hatukustahili. Tunatakiwa kuonyesha upendo kwa Mungu kwa hali zote..

Yesu alisema, amri ya pili ni kupenda jirani yako vile unajipenda. Tunaonyesha upendo kwa Mungu kwa kupenda wenzetu. Upendo si kwa hiari – ni amri. Upendo si kama unajisikia – lazima ionyeshwe kwa wenzetu kwa vitendo. Upendo ni kuwa wazuri kwa wenzetu hata kama si wazuri kwetu. Upendo ni kuweka wenzetu kwanza.

**Furaha**
Tukitubu na tubatizwe, kunakuwa na furaha mbinguni. Tena tufurahi kwa sababu tuko wamoja kwa familia ya Mungu. Tunatakiwa tuwe na furaha mioyoni mwetu hata kama kuna nini, kwa sababu Mungu yuko pamoja nasi tena anatujali. Tunatakiwa tutarajie Ufalme wa Mungu na furaha.

Paulo na Sila waliimbia Mungu nyimbo na hali walikuwa wamepigwa na kuwekwa gerezani. Walikuwa na maumivu na hatari lakini walikuwa na furaha kwa sababu walijua Mungu anawalinda. Yesu alivumilia mateso na maumivu ya msalaba kwa furaha kwa sababu alitarajia kwenda kwenye Baba yake ako.

**Amani**
Yesu ni amani yetu. Alidhihirisha amani kwa kutoa uhai wake usiokuwa na mawaa kama dhabihu ili dhambi zetu zisamehewe. Alitusaidia sisi tuwe na amani na Mungu. Lazima tuishi na amani katikati yetu. Lazima tuwe wapatanishi. Tusigombane na wenzetu, lakini tujaribu kuishi na amani na kila mtu.

**Uvumlivu**
Kwa mateso ya Ayubu yote aliyavumilia. Mwishowe Mungu alimzawadisha kwa huo uvumilivu. Lazima tujifunze kuwa na uvumilivu tukiwa na mateso. Lazima tuangazie kwa Ufalme na kwa uvumilivu tuutarajie. Tena tuvumilie wenzetu. Saa zingine inakuwa vigumu kuvumilia mtu anayeudhi au mzumbuvu au wa kiburi. Tunatakiwa tukumbuke mfano wa Yesu. Wakati watu walimdhihaki na kusema mambo mabaya na ya uongo kwake, alivumilia na hakuwajibu.

**Utu wema**
Utu wema unafanya mabadiliko. Mtu akiwa mwema kwetu anatupa moyo. Kila mara Yesu alikuwa mwema. Aliambia wanafunzi wake wafanyie wenzao chenye wangependa wafanyiwe. Tukijifunza kuona wenzetu vile tujionavyo sisi wenyewe, itakuwa rahisi kuwaelewa na kuwa wema kwao. Lazima tukumbuke wema wa Mungu kwetu na sisi tuwe wema kwa wenzetu.

**Fadhili**
Mungu ni mzuri kweli. Kuwa wazuri kwa maisha yetu lazima tusiwe wachoyo wala watenda dhambi. Tunatakiwa tujaze mawazo yetu na mambo kutoka kwa neno la Mungu. Paulo anatupa wasia mzuri kwa Wafilipi 4:8.

**Uaminifu**
Baada ya ubatizo, lazima tuanze maisha mapya katika Kristo. Lazima tuishi na imani mpaka mwisho wa maisha yetu. Lazima tumtii Mungu kila wakati na tuwe na imani kwake. Ni lazima atatulinda kwa imani.

**Upole**
Lazima tuwe wapole kwa wenzetu. Lazima tusiwe watu wakali au wa kubishana lakini tuwe wapole tukihimiza wenzetu wawe vivyo hivyo bila kugombana.

**Kiasi**
Mtu mbaya sana kusimamia ni wewe mwenyewe. Hii haikui kwamba ni asili. Kila mtu ana dhambi fulani yenye inakuwa vigumu sana kushinda. Tukitaka kuingia kwa Ufalme wa Mungu ni lazima tujifunze kujizuia na tushinde.

**Tunda la roho** ni tabia za Mungu kukua ndani ya maisha ya watu wanaofanya kazi wakisaidiwa naye. Kukua na uonyeshe hili tunda la roho ni kujifunza kupenda, kufurahi, kuwa na amani, kuvumilia,kuwa mwema, kufadhili, kuamini, kuwa mpole na kuwa kiasi. Ni jambo la milele. Tunapigania kuwacha kujipenda sisi wenyewe, badala yake tupendeze Mungu. Wakati wote Mungu Ako, anafanya kazi kwa maisha yetu, akisaidia juhudi letu.